**HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE.**
**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KITUO RAFIKI CHA VIJANA (ANGAZA) TAREHE 27/07/2017.**

**WAJUMBE.**

| S/N. | JINA KAMILI | KATA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Wallace Mashanda | Nyaishozi | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mh. Dawson .P. Byamanyirwohi | Rugera | Mjumbe |
| 3. | Mh. Jovitha Kombe | V/M Nyabiyonza | Mjumbe |
| 4 | Mh. Fideli B. Mugabo | Bweranyange | Mjumbe |
| 5. | Mh. Jane A. Bilaro | V/M Nyaishozi | Mjumbe |
| 6. | Mh. Prisca .K. Busenene | V/M Kibondo | Mjumbe |
| 7. | Mh. Genegeva J. Kanyiginya | V/M Kituntu | Mjumbe |
| 8. | Mh. Magnus Kamugisha Cheusi | Kibondo | Mjumbe |
| 9. | Mh. Zidina T. Murushid | Kituntu | Mjumbe |
| 10. | Mh. Charles B. Beichumila | Nyakahanga | Mjumbe |
| 11. | Mh. Joyce M. Aenda | V/M Kayanga | Mjumbe |
| 12. | Mh. Justin T. Fidelis | Nyakabanga | Mjumbe |
| 13. | Mh. Evalista Sylivesta | Kiruruma | Mjumbe |
| 14. | Mh. Josephat B. Kinyina | Nyabiyonza | Mjumbe |
| 15. | Mh. Adrian R. Kobushoke | Rugu | Mjumbe |
| 16. | Mh. Edward E. Mpaka | Ndama | Mjumbe |
| 17. | Mh. Wilbard R. Abdallah | Igurwa | Mjumbe |
| 18. | Mh. Vaileth J. Kakuba | V/M Nyabiyonza | Mjumbe |
| 19. | Mh. Mzakiru Mussa | Kamagambo | Mjumbe |
| 20. | Mh. Leonard K. Ruhuna | Chanika | Mjumbe |
| 21. | Mh. Felix R. Mkuchu | Ihembe | Mjumbe |
| 22. | Mh. Xavery F. Buguzi | Nyakakika | Mjumbe |
| 23. | Mh. Adventina C. Kahatano | Kayanga | Mjumbe |
| 24. | Mh. Rwamuhangi S. Mugasha | Kayanga | Mjumbe |
| 25. | Mh. Aneth K. Bagonza | V/M Kihanga | Mjumbe |
| 26. | Mh. Novart Kishenyi | Chonyonyo | Mjumbe |
| 27. | Mh. Vallace R. Kasumuni | Nyakasimbi | Mjumbe |
| 28. | Mh. Aristides. B. Muliro | Bugene | Mjumbe |
| 29. | Mh. Joackim January | Ihanda | Mjumbe |
| 30 | Mh. Sabby Rwazo | Kanoni | Mjumbe |
| 31. | Mh. Innocent Bashungwa | Mbunge- jimbo la Karagwe | Mjumbe |
| 31 | Ndg. Godwin M. Kitonka | Mkurugenzi Mtendaji | **Katibu** |

**WATAALAM.**

| S/N | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Kiwango R. A. | Kaimu, Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 2 | Ndg. Jackson Mwakisu | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 3 | Ndg. Paschal Thomas | Mkuu wa Chuo KDVTC |
| 4 | Ndg. Innocent Mwalo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 5 | Ndg. Edina Kabyazi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii |
| 6. | Ndg. Ashura Kajuna | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 7. | Ndg. Kulwa Mkwama | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 8. | Ndg. Adam Salum | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushiirika |
| 9. | Ndg. Bernard Essau | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 10. | Ndg. P. R. Rweyendera | Mkuu wa Idara ya Mazingira na usimamizi wa taka ngumu |
| 11. | Eng. Ludovick Mtagurwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 12 | Ndg. Edius Rwangoga | Mratibu TASAF |
| 13. | Ndg. Rajab Khasimu | Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 14. | Ndg. Upendo Rweyemamu | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 15. | Ndg. Donati Bunonosi | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 16 | Eng. Wolta Kirita | Mkuu wa Idara ya Maji |
| 17 | Ndg. Benjamin Kawamala | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 18 | Ndg. Anita Constatine | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi |
| 19 | Ndg. Peter K. Evarister | Afisa Biashara |
| 20 | Ndg. Beatrice Laurent | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya |
| 21 | Ndg.Robert Mugendi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi |
| 22 | Ndg. Devotha Tibanywana | Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Kayanga |
| 23 | Ndg. Wilking Shuma | Meneja maji Mjini |
| 24. | Ndg. Moris Muliro | Mtakwimu |

**WAALIKWA.**

| S/N | JINA KAMILI | WADHIFA/ANAKOTOKA |
|---|---|---|
| 1. | Mh. Mustafa S. Kijuu | Mkuu wa Mkoa Kagera |
| 2. | Mhe. Godfrey Mheluka | Mhe. Mkuu wa Wilaya |
| 3 | SSP. Boaz Rugayi | D.P.O |
| 4. | Ndg. Innocent Nsena | Katibu tawala (W) |
| 5 | Ndg. Robinson Mutafungwa | M/Kiti CCM (W) |
| 6 | Ndg. Mary H. Kamanda | Katibu CCM (W) |
| 7. | Ndg. Jovinus Ezekiel | Radio KARAGWE |
| 8. | Ndg. Rashida Mfaume | For. DCB |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Ndg. Ivo Ndisanye | Katibu wa Mbunge |
| 10. | Ndg. Romanus Msafiri | DSO |
| 11. | SSP. Mika Makanja | OCD – Karagwe |
| 12 | Cpt. S. K. Hango | MJA |
| 13 | Ndg. Ellen Magambo | Redio KWIZERA |
| 14 | Ndg. Leopold Ngirwa | Mkaguzi wa Ndani-RS |
| 15. | Ndg. Costantine Mabirika | Mkaguzi Mkuu wa Nje-NAO |
| 16. | Ndg. Pius Ngaiza | FMO-RS |
| 17. | Ndg. Rajab A. Kiravu | Mkaguzi wa Nje-NAO |
| 18. | Ndg. Thomas James | Katibu wa RC |
| 19. | Ndg. Athuman Hussein | Mlinzi wa RC |

**MAAFISA TARAFA**

| S/N | JINA KAMILI | TARAFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Erasto Hajanja | Nyabiyonza |
| 2. | Ndg. Medard Baletwa | Nyaishozi |
| 3. | Ndg. Nyangele Makunenge | Kituntu |
| 4 | Ndg. Rozalia Njiani | Bugene |
| 5. | Ndg. Gratian Kikabiha | Nyakakika |

**SEKRETARIETI.**

1. Wilson Byarugaba
2. Joyce Kitundu

**DONDOO**

1. Kufungua kikao
2. Kupokea salamu kutoka Serikali Kuu
3. Kujadili Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Halmashauri zilizoishia tarehe 30 Juni 2016.
4. Kufunga Kikao

**KUMB. NA. 100/2016/2017/9 - KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao Katibu aliwakaribisha wajumbe na kufanya utambulisho kwa wageni waliohudhuria toka Mkoani.

Akifungua kikao Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na wageni walioalikwa na kuwataka kuchangia kwa makini mawazo yao ili kufanikisha kikao.

Alipongeza Menejimenti na Waheshimiwa Madiwani pamoja na uongozi wa Wilaya kwa kuendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

Alipongeza Menejimenti, Waheshimiwa Madiwani na wadau wengine kwa ushirikiano uliwezesha Halashauri kupata Hati inayoridhisha na aliionesha kwa wajumbe.

Alisisitiza kuwa Hoja za Ukaguzi zinachangiwa na baadhi ya changamoto ikiwa ni pamoja na upungufu uliokithiri wa watumishi na  upungufu wa rasilimali fedha.

Aliipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili yaujenzi wa  Kituo cha Afya Kayanga ambao unaendelea.

Kikao kilifunguliwa mnamo saa 5:37 asubuhi.

**KUMB. NA. 101/2016/2017/9 - KUPOKEA SALAMU KUTOKA SERIKALI KUU**

Akimkaribisha Mgeni rasmi, Mhe. Mkuu wa Wilaya aliishukuru Serikali kwa fedha za ujenzi wa kituo cha Afya Kayanga. Aidha aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani na wadau mbalimbali kwa utekelezaji wa majukumu ya kila siku na miradi ya maendeleo.

Akitoa salamu zake Mhe. Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Kagera alieleza kuwa kikao hiki ni mwendelezo wa Agizo la Mhe. Rais likifuatiwa na maelekezo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI  kuwa Kila Mkuu wa Mkoa ahakikishe anashiriki kikamilifu katika kikao maalum cha kujadili Hoja za CAG na kutoa ushauri na maagizo juu ya hoja zinazojitokeza.

Aliipongeza Menejimenti, watumishi na Waheshimiwa Madiwani kwa utendaji kazi mzuri uliowezesha Halmashauri kupata **Hati ya Kuridhisha** kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2016 tofauti na mwaka uliopita ambapo Halmashauri ilipata Hati ya Mashaka.

Alibainisha baadhi ya kasoro zilizojitokeza katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016 ikiwa ni pamoja na utekelezaji hafifu wa hoja za miaka ya nyuma na maagizo ya Kamati ya Bunge, ukusanyaji mdogo wa mapato, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokamilika kwa wakati na kutumia

fedha za miradi tofauti na miradi iliyoidhinishwa, usimamizi wa mikataba na upelekaji wa fedha za mfuko wa wanawake na vijana usiokamilika kama ilivyoagizwa.

Baada ya kuainisha changamoto hizo alitoa **maagizo** kama ifuatavyo.

- Utekelezaji wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Seikali, inakuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya Menejimenti na vikao vya Kamati ta Fedha, Uongozi na Mipango.
- Kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa Ndani inaimarishwa kwa kuwatumia kikamilifu wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri katika kufanya tathimini ya ufanisi wa mifumo yote ya Halmashauri na kuchukua hatua stahiki
- Kamati ya Ukaguzi iwezeshwe kikamilifu ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.
- Halmashauri ibuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mapato ya ndani pia kuhakikisha mfumo wa kielektroniki wa kukusanya Mapato unafanya kazi kikamilifu.
- Menejimenti kufanya uchambuzi wa mikataba yote na kubainisha mikataba yenye vipengele vinavyoweza kuathiri maslahi ya Halmashauri na kuchukua hatua stahiki, ikiwemo kurekebisha vipengele hivyo kwa kusingatia ushauri utakaotolewa na Katibu Tawala wa Mkoa.
- Mfuko wa wananwake na vijana utengewe fedha kama inavyoelekezwa.
- Kuchukua hatua za kimidhamu na kisheria zilizochukuliwa kwa watumishi na wote waliosababisha kwa namna yoyote kasoro zilibainika katika ukaguzi na taarifa itolewe kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

**Salamu kutoka kwa Mhe. Mbunge.**

Akitoa salamu aliipongeza Serikali kwa kutoa fedha za miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwemo mradi Kituo cha Afya Kayanga. Alitoa ombi kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa juu ya ufuatiliaji wa taratibu zinazotakiwa kufuatwa ngazi ya Mkoa, ili kuomba vibali kwa ajili ya kufunguliwa kwa Zahanati za Ihembe, Rubare na Kategire. Aidha alitoa taarifa ya watumishi wapatao 152 waliopo Hospitali ya Nyakahanga kutopokea mishahara kwa kipindi cha miezi mitatu.

Alitoa ombi kwa Serikali ya Mkoa kuruhusu kupatiwa leseni Wilayani badala ya Mkoani kwa madereva wa 'bodaboda'.

Kuhusu upungufu mkubwa wa watumishi hususani kwa Idara za Afya na Elimu alitoa ombi kwa Serikali kufikiria jambo hilo ili kuwezesha shughuli za Serikali kuendelea kufanyika kwa ufasaha.

Aliipongeza Shule ya Sekondari Bugene kwa kushika nafasi ya nne ngazi ya Mkoa katika ufaulu wa kidato cha sita, na kuomba Serikali isaidie ujenzi wa Maktaba ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

**KUMB. NA. 102/2016/2017/9 - KUJADILI HOJA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA HALMASHAURI ZILIZOISHIA TAREHE 30 JUNI 2016.**

Hoja 2.1.1 - kuhusu ufanisi katika mapato
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa Halmashauri iongeze mashine za POS ili kudhibiti na kuongeza mapato ya ndani.

Hoja na 2.1.1 (b) – kuhusu fedha za matumizi ya kawaida
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.1.2 - ufanisi katika masuala ya matumizi
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja na 2.1.2 (b) kuhusu matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.2.1 kuhusu ukaguzi wa taarifa za fedha.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.2.2 kuhusu madeni (wadai) ya muda mrefu TSh. 1,046,569,000/=
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.2.3 kuhusu malinganisho ya muda mrefu katika taarifa za usuluhishi wa benki.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.3.1 kuhusu mashauri yaliyoko mahakamani
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.4.1 kuhusu Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.5.1 kuhusu Menejimenti ya Rasilimali watu na Mishahara
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.5.2 kuhusu Mishahara iliyohamishiwa BoT moja kwa moja toka akaunti za Watumishi na hakuna stakabadhi ya kukiri mapokezi toka kwa Mlipwaji TZS. 23,261,120.00
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.5.3 kuhusu Malipo ya Mishahara kwa Watumishi ambao ajira yao Serikalini ilisha hitimishwa TZS. 57,035,150.00
Maoni ya Baraza-wajumbe **waliagiza** Menejimenti iendelee kufanya ufuatiliaji ili fedha hizo zirejeshwe.

Hoja 2.6.1 kuhusu masuala ya utawala
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.7.1 kuhusu Mafuta yaliyotumika katika magari bila kuandikwa katika vitabu vya magari husika TZS. 2,570,560.
Maoni ya Baraza-wajumbe **waliagiza** ufuatiliaji uendelee na hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe.

Hoja 2.8.1.1 kuhusu Udhaifu ulioonekana katika matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Makusanyo ya Mapato ya Serikali za Mitaa
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.8.1.3 kuhusu Mapato amabayo hayajathibitishwa kupelekwa Benki TZS.1,546,100.00
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja2.8.2.1 kuhusu Fedha iliyokopwa katika akaunti ya Amana kwa ajili ya kulipa matumizi ya kawaida isiyorejeshwa – TZS 27,572,817
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.8.2.2 kuhusu Malipo yaliyofanyika katika akaunti ya Amana bila kutaja stakabadhi husika iliyoweka fedha hizo – TZS 194,867,120
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza Menejimenti kusimamia utunzaji wa nyaraka zote za Serikali.

Hoja 2.8.2.3 kuhusu Masurufu yasiyorejeshwa – TZS 35,899,510
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza Menejimenti kusimamia urejeshwaji wa masurufu ndani ya siku 14 zilizoainishwa kisheria.

Hoja 2.8.2.4 kuhusu Kukosekana kwa hati za Malipo – TZS 11,136,901
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.8.2.5 kuhusu Matumizi ya fedha ambayo vielelezo havijitoshelezi – TZS 90,802,576
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa wazabuni waelimishwe kuwasilisha risiti za mapokezi ya fedha kabla ya kukabidhwa fedha zao.

Hoja**2.8.2.6** kuhusu Matengenezo ya gari (SM 3495) yalifanyika kwa fedha taslimu kwa mtu binafsi, bila kupata idhini kutoka TEMESA – TZS 5,313,000/-
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja **2.8.2.7** kuhusu Fedha za Afya na Elimu zilipokelewa katika akaunti ya Matumizi Mengine hazikuhamishwa kwenda kwenye akaunti husika – TZS 64,063,000
Maoni ya Baraza- wajumbe **waliazimia** kuwa mchanganuo wa fedha hizo uwasilishwe kwenye kikao kijacho cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

Hoja **2.8.2.8** kuhusu Kutohamishwa kwa fedha za Posho ya kuitwa kazini kutoka akaunti ya Sekta ya Afya – TZS 19,101,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja **2.8.2.9** kuhusu Fedha za Posho ya kuitwa kazini imelipwa zaidi ya fedha zilizohamishwa kwa TZS 11,959,000
Maoni ya Baraza- wajumbe **waliagiza** ufuatiliaji ufanyike na taarifa itolewe kikao kijacho cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

Hoja 2.8.2.10 kuhusu Kutumia fedha za Likizo kiasi cha TZS 8,826,800 kwa matumizi mengine bila kuomba idhini pamoja na kuwepo kwa madai ya likizo ambayo hayakulipwa yenye thamani ya TZS 11,974,600
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.8.2.11 kuhusu Kutumia fedha za Mitihanai ya Sekondari kwa kazi nyingine bila kupata idhini kutoka Kamati ya Fedha na Hazina/Ofisi ya Rais – TAMISEMI – TZS 22,870,970.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha.

Hoja 2.8.2.12 kuhusu Stahiki ya Samani kulipwa nje ya Bajeti – TZS 14,000,000 na Stahiki ya Simu kulipwa kwa afisa asiyestahili – TZS 6,790,000
Maoni ya Baraza- wajumbe **waliagiza** kuwa fedha hizo zirejeshwe kabla ya mwezi wa nane.

Hoja 2.9.1.1 kuhusu Kutoletwa kwa fedha za Ruzuku ya Miradi ya Maendelo (LGCDG) – TZS 587,536,366
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

**HOJA ZINGINE**

Hoja 2.10.1.1 kuhusu Mradi wa Umwagiliaji (DIDF) Kutotumika kwa fedha – TZS 184,000,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.2.1 kuhusu Mradi wa Kuthibiti Ukimwi – NMSF Mapitio ya taarifa za Fedha
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.3 kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.4.2 kuhusu Mpango Maalum wa Elimu ya Sekondari awamu ya II (MMES II) - SEDP II Kukosekana kwa hati miliki za maeneo kwa shule za Sekondari Nyakasimbi, Ruhinda, Kawela na Nyakasimbi
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.5.1 kuhusu Mchango pungufu katika Mfuko wa Wanawake na Vijana – TZS 86,437,400
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.5.2 kuhusu Mikopo isiyorejeshwa ya vikundi vya Wanawake na Vijana – TZS 59,805,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

**HOJA ZA MIAKA YA NYUMA**

Hoja 2.2.5.3 - 2011/12 kuhusu Kuchelewa kwa huduma ya ujenzi wa mradi wa umwagiliaji Mwisa
TZS. 586,037,278/=
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza Mkandarasi alipwe malipo yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwakuwa aliwekwa kwenye bajeti.

Hoja 2.2.6.4 - 2011/12 kuhusu Kutokusanya asilimia 20% ya Kodi ya ardhi TZS.3,419,555/=
Maoni ya Baraza- wajumbe **waliagiza** kuwa barua ya kudai hizo fedha iandikwe na kutumwa kukumbushia

Hoja 2.2.7.7 2011/12 kuhusu Kutorejeshwa kiasi cha TZS. 4,023,800 katika Akaunti ya Amana.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.2.7.10 2011/11 kuhusu Matumizi yasiyofaa katika miradi ya maendeleo TZS.690,141,741
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa stakabadhi hizo zionekane ili zipitiwe na wakaguzi.

Hoja2.2.7.11 - 2011/12 kuhusu Kodi (VAT) iliyolipwa katika mradi wa kilimo uliyosamehewa kodi – TZS.10,548,671
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.2.8.1 -2011/12 kuhusu Kutorejesha Hazina mishahara ambayo haikulipwa TZS. 17,071,777
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.9.2 - 2012/13 kuhusu Kukosekana kwa stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka Hazina kwa mishahara ambayo haikulipwa TZS. 68,632,114
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza ufuatiliaji uendelee kufanyika ili stakabadhi husika zipatikane.

Hoja2.3.10.1-2012/13 kuhusu Kukamilika ofisi ya Mbunge wa karagwe, lakini bado haijaanza kutumika
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.13.3-2012/13 kuhusu Kutokamilika ukarabati wa mradi wa maji Kakiki TZS.21,000,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.13.4-2012/13 kuhusu Kutokamilika ujenzi wa nyumba (moja kwa mbili) katika chuo cha ualimu Karagwe TZS.41,000,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.10.1- 2012/13 kuhusu Mchango wa 20% wa Halmashauri kwenda Vijijini kutohamishwa kiasi cha TZS. 25,607,246
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.15.3.1-2012/13 kuhusu Kiasi cha TZS. 311,298,654 mchango wa Halmashauri katika mfuko wa wanawake na vijana kutolipwa.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.13.2- 2012/13 kuhusu Salio la mikopo ya Wanawake na Vijana kiasi cha TZS. 18,080,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.3.15.5- 2012/13 kuhusu Uhamisho wa fedha ya Ruzuku TZS. 57,887,500 kwenda Shule za Msingi kutothibitishwa
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.1.1-2013/14 kuhusu Kutokuwepo uhakika wa kupeleka Benki kiasi cha Tzs 19,523,000/=
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.2.2- 2013/14 kuhusu Fedha zilizokopwa toka akaunti ya amana tzs 115,514,626/= bila kurejeshwa hadi wakati wa ukaguzi
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.8.1- 2013/14 kuhusu Mishahara ambayo haikulipwa (Unclaimed salaries) kutorejeshwa Benki kuu Kiasi cha TZS 32,053,167.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.9.1-2013/14 kuhusu Ufanisi katika miradi ya -(LGCDG). Kutorejesha kiasi cha TZS 223,088,320 katika mfuko LGCDG.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.10.1.1-2013/14(ASDP) kuhusu Kuchelewa kununuliwa kwa mashine ya kukoboa kahawa na ujenzi wa nyumba ya mashine – TZS 124,905,960
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.10.3.1-2013/14(HBF) kuhusu Matumizi yasiyoidhidhinishwa ya fedha za Mfuko wa pamoja wa Afya (Basket Fund) zilizokuwa kwenye akaunti ya Miradi ya Maendeleo – TZS 76,894,325
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.10.3.2-2013/14(HBF) kuhusu Kuletwa kwa dawa na vifaa tiba pungufu zilizonunuliwa kutoka MSD – TZS 19,236,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa vielelezo husika viwasilishwe kwa wakaguzi ili hoja ifungwe.

Hoja 3.3.10.2-2013/14 kuhusu Kutorejesha matumizi ya kiasi cha TZS14,351,900 katika mfuko wa afya ya jamii (CHF).
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.10.4- 2013/14 kuhusu Asilimia 10% za makusanyo ya ndani kiasi cha TZS 90,231,700 kutopelekwa katika mfuko wa Vijana na kinamama.
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza Menejimenti ioneshe upelekaji wa fedha hizo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wakaguzi ili kuomba kufuta hoja hiyo.

Hoja3.3.10.5- 2013/14 kuhusu Mikopo isiyojeshwa katika mfuko wa Wanawake na Vijana – TZS 18,162,200
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 3.3.11.1-2013/14 kuhusu Upungufu wa Miundombinu shuleni
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.5.2- 2014/15 kuhusu Magari yasiyotengenezeka kukaa muda mrefu
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.7.1- 2014/15kuhusu Upungufu wa watumishi 1,191 katika Halmashauri ya wilaya ya Karagwe
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.7.2- 2014/15 kuhusu Mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufa ama kuacha kazi TZS 9,340,960
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa wahusika warejeshe fedha hizo, aidha wakikaidi wachukuliwe hatua za kisheria.

Hoja 2.9.1.1- 2014/15 kuhusu Mapungufu yaliyobainishwa kwenye mfumo wa Kihasibu.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.9.1.4.1-2014/15kuhusu Tofauti iliyojitokeza kati ya mafuta yaliyopokelewa idara ya Afya na kiasi kilichoingizwa kwenye leja.
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa wahusika wawasilishwe vielelezo ili hoja ifungwe.

Hoja 2.10.1.1-2014/2015 kuhusu Makusanyo ya ushuru wa ardhi hayakupelekwa Wizara ya Ardhi – TZS 35,392,639
Maoni ya Baraza- wajumbe **waliazimia** kuwa Halmashauri irejeshe fedha hizo Wizarani kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ili ianze mkakati wa kudai Wizara ruzuku zinazotakiwa kurejeshwa tena Halmashauri.

Hoja 2.10.1.2-2014/2015 kuhusu Kodi ya Ardhi haikupokelewa kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - TZS.25,452,682
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.1.3-2014/2015 kuhusu Wakati wa Ukaguzi kitabu kimoja hakijapatikana.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.1.4-2014/2015 kuhusu Mapato ambayo hayajakusanywa kutoka kwa Mawakala wa Mapato wa Halmashauri - TZS.16,906,157.00
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.10.2.3-2014/2015 kuhusu Malipo nje ya bajeti TZS. 7,009,000.00
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.11.1.1-2014/2015 kuhusu Kutojulikana na Matumizi ya fedha za SEDP kiasi cha TZS.90,624,621
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja2014/2015 (**ROAD FUND)** (a) kuhusu Malipo yaliyofanyika kwa mtu mwingine tofauti na Jina la Mzabuni lililosajiliwa – TZS 13,923,804
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja Hoja2014/2015 (**ROAD FUND)** (b) kuhusu Upungufu wa Watumishi 15 katika Idara ya Ujenzi
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja2014/2015(**ASDP)** (a) kuhusu Mapungufu yaliyobainishwa katika mkataba wa ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba ya watumishi katika kituo cha Kilimo cha Kata ya Bweranyange – TZS 29,926,886
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja2014/2015(**ASDP)** (b)kuhusu Upungufu wa Watumishi 126 katika Idara ya Kilimo
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2014/2015(**HBF) (a)** kuhusu Nyaraka za mikataba hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi – TZS 8,003,365 Halmasahuri inasisitizwa kuandaa na kuwasilisha majibu kwa ajili ya uhakiki
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2014/2015(**HBF) (b)** kuhusu Kazi zilizopangwa hazikufanyika pamoja na kupokelewa kwa fedha zote – TZS 17,669,583 Halmasahuri inasisitizwa kuandaa na kuwasilisha majibu kwa ajili ya uhakiki
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.12.3.1-2014/2015 kuhusu Fedha zilizokopwa kwa ajili ya kuendesha zoezi la uchaguzi Mkuu wa Serikali za Mitaa 2014 zisizorejeshwa kiasi cha TZS.32,634,179
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.12.4.1-2014/2015 kuhusu Halmashauri kutochangia kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana kutokana na Mapato yake ya ndani – TZS 16,282,423
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja2.12.4.2-2014/2015 kuhusu Mikopo inayodaiwa vikundi vya akina Mama na Vijana - TZS.7,810,000
Maoni ya Baraza- wajumbe walishauri kuwa elimu juu ya dawati la uwezeshwaji ngazi ya Wilaya itolewe katika kikao cha Baraza lijalo ili wajumbe wapate uelewa wa pamoja.

Hoja 2.12.5.1-2014/2015 kuhusu Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara kutokamilika ndani ya muda uliopangwa
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.12.5.2-2014/2015 kuhusu Upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na mafundi sanifu (Science Teachers & Laboratory Technicians)
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.12.5.3-2014/2015 kuhusu Vifaa vya ujenzi wa maabara vilinunuliwa zaidi ya mahitaji - TZS.14,088,979/=
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 2.12.62014/2015-kuhusu Upungufu wa miundombinu ya shule.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

## MAAGIZO YA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)

Hoja 2 kuhusu Uongozi wa halmashauri kuhakikisha kiasi cha TZS 566,088,999/= ambacho hakijahamishwa katika mfuko wa Vijana na wanawake na kiasi cha TZS 25,607,247/= asilimia 20% za vijiji kwa mwaka wa fedha 2013/2014.
Maoni ya Baraza- wajumbe walisisitiza kuwa fedha ya mfuko wa wanawake na vijana iwe inatengwa yote kama ilivyoelekezwa. Aidha Menejimenti ioneshe mchanganuo namna ilivyopeleka fedha hizo kwa mwaka 2016/2018 ili kuomba hoja ifungwe.

Hoja 3 kuhusu Uongozi wa Halmashauri kuchukua hatua za makusudi kujenga uwezo katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mawakala.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 4 kuhusu RAS-Kagera kushirikiana na uongozi wa Halmashauri kufuatilia fedha ambazo hazikupokelewa na Halmashauri – TZS 73,228,800
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 5 kuhusu Uongozi wa Halmashauri kufuatilia fedha za uuzaji wa magari ambayo yalikuwa katika yadi ya Halmashauri.
Maoni ya Baraza- wajumbe **waliazimia** kuwa mhusika awasilishe vielelezo ndani ya siku 14.

Hoja 7 kuhusu Uongozi wa Halmashauri uhakikishe ujenzi wa umwagiliaji Mwisa unakamilika na kamati ya Bunge LAAC wanatembelea mradi huo kabla ya mwezi wa kwanza, 2014.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 9 kuhusu Uongozi wa halmashari kurejesha kiasi cha TZS 365,141,741 ambazo zilitumika kinyume cha sheria, kwa kuombea kibari cha kuharalisha sha matumizi hayo kutoka baraza la Madiwani. Na kutuma nyaraka za marejesho ya fedha katika ofisi ya mkaguzi kwa uhakiki.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja 10 kuhusu RAS-Kagera kwa kushiriakana na Wizara ya fedha Hazina kufuatilia kiasi cha fedha TZS 200,000,000/= ambazo hazikupokelewa na Halmashauri ya wilaya ya Karagwe, na kutuma vielelezo kwa mkaguzi mkazi kwa uhakiki.
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Hoja kuhusu Uongozi wa Halmashauri kuwasirisha nyaraka kwa mkaguzi mkazi za urejeshaji Hazina mishahara ambayo haijalipwa (unclaimed salaries) kiasi cha TZS 17,071,777/=
Maoni ya Baraza- wajumbe walikubaliana na majibu ya Menejimenti na maoni ya Kamati ya Fedha

Baada ya jupitia hoja zote Mhe. Mkuu wa Mkoa **aliagiza na kusisitiza** yafuatayo;

1. Wahusika wote wa hija waainishwe na Hoja zote zijibiwe kwa wakati.
2. Hoja zote za miaka ya nyuma zifuatiliwe na zijibiwe kikamilifu ili hoja zifungwe ndani ya miezi sita.
3. Wakaguzi wa Ndani watumike vema kukagua malipo yote kila mwezi, aidha Kamati ya Ukaguzi iwezeshwe ili kutekeleza shughuli zake kikamilifu
4. Mapato yote ya Halmashauri yakusanywe kwa POS
5. Mapato yote ya Halmashauri yaingizwe Benki kabla hayatumika
6. Halmashauri ibuni vyanzo vingine vya mapato ili kuongeza mapato ya ndani

7. Miradi ya maendeeleo isimamiwe na ikamilike kwa wakati.
8. Mikataba isiyo na maslahi kwa Halmashauri ipitiwe upya na irekebishwe kulingana na maslahi ya Halmashauri, kwa ushauri wa Katibu Tawala wa Mkoa.
9. Fedha za mfuko wa wanawake na vijana zipelekwe kama ilivyoelekezwa na Menejimenti ibuni namna bora ya kukopesha vikundi ili wanufaike na mikopo hiyo.
10. Wananchi waelimishwe kuhusu Dawati la Uwezeshwaji
11. Kuhusu uuzaji wa magari chakavu Menejimenti iendelee kufanya ufuatiliaji kwa wahusika kwa utekelezaji wa haraka.

**KUMB. NA. 103/2016/2017/9 –KUFUNGA KIKAO**

Akifunga kikao Mwenyekiti kutekeleza maagizo yote na kufuata ushauri uliotolewa ili kufungwa na kutojirudia kwa Hoja. Alitoa ombi kwa Serikali kujaza nafazi za Wakuu wa Idara waliohama.

Kikao kilifugwa mnamo saa 10:10 jioni.

| | |
|---|---|
| Ndg. Godwin M. Kitonka | Mh. Wallace Mashanda |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**Umethibitishwa leo………………………………..**

aliwapongeza wajumbe na wadau wote kwa kufanikisha kikao. Alisisitiza Menejimenti